BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Nne – Tarehe 19 Februari, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

14. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Kwa kuwa Serikali inaendelea na zoezi la kuongeza gharama za matumizi kwa maeneo mengi, na kwa kuwa gharama za matumizi zinaongezeka siku hadi siku, na kwa kuwa miaka mingi imepita bila ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kuongezwa.

    Je, ni lini Serikali itaongeza fedha za Mfuko huo ili kuwanufaisha zaidi wananchi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

38. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni jambo la kupongezwa kwamba Serikali, kupitia miradi ya Baraza la Mji Wete, imekusudia kujenga soko la kisasa katika shehia ya Mzambarauni ndani ya jimbo la Pandani. Hata hivyo, kumekuwa na taarifa zilizoripotiwa katika kipindi cha Mawio kupitia ZBC Radio kwamba kuna viongozi wamepinga ujenzi huo katika vikao vya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

(a) Je, ni Kiongozi gani na katika kikao kipi cha Baraza au nje ya Baraza kumepingwa Ujenzi wa Soko la Mzambarauni.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kupitisha na kutekeleza miradi ya Baraza la Mji Wete.

(c) Je, ni yapi mamlaka ya viongozi wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika kupitisha na kutekeleza miradi ya Baraza la Mji Wete.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

112. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Moja ya faida kubwa ya uwekezaji katika nyanja mbali mbali za kiuchumi ni kupatikana kwa ajira binafsi nchini.

Tathmini iko vipi hususani kwa wazawa katika kuona kwamba wanafaidika na fursa ya uwekezaji nchini.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

25. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) limeingia mikataba ya kutoa huduma za bima kupitia mawakala na mabenki mbali mbali hapa nchini.

(a) Je, ni benki zipi zilizoingia katika mkataba huu wa kutoa huduma za bima.

(b) Je, ni upi muitiko wa wananchi wa kuzifikia benki hizo katika kufuata huduma hiyo.

142. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kufuatia ripoti ya Disemba, 2023, Shirika la Fedha Duniani (IMF) kuiweka Tanzania kwenye orodha ya nchi zenye mfumo dhaifu wa utakatishaji fedha na ufadhili wa kigaidi:

(a) Je, ni athari zipi hasa ambazo Zanzibar inaweza kuzipata baada ya Tanzania kuwekwa katika orodha ya kijivu na Kikosi Kazi cha Ukaguzi wa Masuala ya Fedha Duniani (FATF).

(b) Je, Serikali ina mipango gani thabiti ya kuhakikisha kwamba Zanzibar, pamoja na Tanzania kwa ujumla, haziathiriki zaidi na hatua hii ya IMF.

(c) Je, baada ya ripoti za IMF na FATF kuonyesha hali isiyotia moyo katika miaka iliyopita, kuna mikakati gani ya Serikali inayolenga kuboresha mifumo yake ya kifedha.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

98. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni maboresho gani ambayo yanalifanya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kuweza kuingia kwenye ushindani kupitia mabadiliko mbali mbali ya vipindi vyake.

99. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Tuna idadi ngapi ya wakufunzi wa mpira wa miguu Zanzibar wenye leseni Grade ‘A’ kutoka CUF.

(b) Kwa kiasi gani wakufunzi hawa, wanatumika ipasavyo katika kuinua soka la mpira wa miguu Zanzibar.

(c) Ni changamoto gani zinazopelekea kuwa na uhaba wa wakufunzi wa ‘Grade A’ katika soka la mpira wa miguu nchini mwetu.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

4. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha Kitengo cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Hata hivyo, bado Serikali haijaimarisha huduma ya afya kwa Watu wenye Ulemavu wa ngozi (Albino).

Je, Serikali imejipanga vipi kuwasaidia Watu wenye Ulemavu wa ngozi (Albino) kwa kuwaangalia afya zao ili kuwakinga na magonjwa mbali mbali kama vile saratani ya ngozi.

135. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Miongoni mwa changamoto mbali mbali zinazowakabili wajawazito ni pamoja na matumizi ya dawa za kienyeji kwa ajili ya kuongeza uchungu.

Je, athari gani huweza kupata mjamzito, anapotumia dawa za kienyeji kwa lengo la kumuongezea uchungu.

<u>**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**</u>

164. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Makumbusho ya Mwinyi Mkuu Dunga ni miongoni mwa maeneo yenye historia halisi ya uwepo wa tawala za kijadi zilizokuwa na nguvu na kuimarika kiuchumi na kiustarabu. Kwa kuwa kwa muda mrefu makumbusho hayo hayajawekewa mazingira halisi kwa muktadha wake.

Je, ni yepi matarajio ya Wizara yako katika kuihuisha historia ya tawala za jadi za Mwinyi Mkuu zilizowahi kuwepo nchini kwetu.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

50. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Awamu ya Nane inastahili pongezi kwa kusimamia uanzishwaji na uzinduzi wa Taasisi ya Teknolojia ya India Madras kupitia mashirikiano ya aina yake (Unique Partnership) kati ya Serikali ya India na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, bado kuna mgongano wa kimaslahi ambao haujakaa sawa kisheria, kiutaratibu na kiutawala.

(a) Je, ni sheria ipi au sehemu ipi ya sheria iliyotumika kuanzisha IIT Madras Kampasi ya Zanzibar.

(b) Je, ni zipi haki, nguvu na dhima ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uendeshaji wa IIT Madras Kampasi ya Zanzibar.

(c) Je, ni kwa kiasi gani matakwa ya Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 imefuatwa au imekiukwa katika uanzishaji wa IIT Madras Kampasi ya Zanzibar.

137. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ingawa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuwasaidia wanafunzi kupata ufadhili, bado kuna changamoto kadhaa zinazoathiri waombaji na wanaonufaika na mikopo hii.

(a) Je, ni ipi takwimu halisi ya idadi ya wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2020-2023).

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kukabiliana na ucheleweshaji unaotokea mara kwa mara katika utoaji wa fedha za kujikimu kwa wanafunzi wanaosoma ndani na nje ya nchi kila wanapoanza muhula wa masomo.

(c) Katika hali ambayo wanafunzi wanapokea sehemu ya mkopo wao kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania (HELB), Serikali inachukua hatua gani kushughulikia suala hili na kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanapata ufadhili unaohitajika kwa mafanikio yao ya kitaaluma.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

49. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali, kupitia kauli mbalimbali za viongozi, imekuwa ikiahidi kuwapatia wananchi, hasa kinamama, vifaa na mikopo nafuu kwa ajili ya uzalishaji bora na wenye tija wa mwani. Hata hivyo, utekelezaji wa azma hiyo haujaenda sambamba na dhamira na kauli za viongozi hasa katika jimbo la Pandani.

(a) Je, ni lini akinamama wa shehia za Shengejuu, Kiungoni na Mjananza zote katika jimbo la Pandani watapatiwa vifaa na mikopo nafuu kwa ajili ya uzalishaji bora na wenye tija wa mwani kama ilivyoahidiwa.

(b) Kwa nini kuna urasimu na usiri mkubwa katika kupatikana vifaa na mikopo nafuu kwa ajili ya uzalishaji bora na wenye tija wa mwani kama ilivyoahidiwa.

(c) Je, ni ipi takwimu ya miaka mitatu (2020/2021 – 2022/2023) ya kupatikana vifaa na mikopo nafuu kwa ajili ya uzalishaji bora na wenye tija wa mwani katika jimbo la Pandani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

83. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kujipatia ajira, wananchi wengi wa jimbo la Paje wanajiendeleza na kilimo cha ndimu, kama zao kuu la biashara.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwatafutia soko la nje ya nchi wakulima hao.

(b) Je, ni lini utawatembelea wakulima hao pamoja na kujionea wanavyolima zao hilo.

(c) Je, unawaambia nini wakulima wa jimbo la Paje kuhusu biashara ya zao la ndimu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

15. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Kwa kuwa baadhi ya maeneo katika jimbo la Wawi kama vile Gombani, Mgogoni, Mkoroshoni na kadhalika yanakabiliwa na changamoto ya kutopata maji ya uhakika, na kwa kuwa huduma ya maji ni miongoni mwa huduma ya msingi katika maisha ya mwananchi.

    Je, ni lini wananchi wote wa jimbo la Wawi watapata huduma ya maji ya uhakika.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

57. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Kumekuwa na matangazo ya vyombo vya baharini vinavyolazimisha nauli za watoto ziwe kwa watoto wasiozidi miaka 10 badala ya miaka 18 ya kimataifa au miaka 12 ya SUMATRA.

    (a) Je, ni ipi mantiki ya kuwa na bei ya mtoto katika vyombo vya usafiri.

    (b) Je, ni sheria ipi inayomtambua mtoto kwamba lazima asizidi miaka 10.

    (c) Je, kwa nini Serikali haizielekezi mamlaka husika kuangalia uwezekano wa kuwa na punguzo la bei katika vyombo vya usafiri kwa wazee waliozidi miaka 70 na wanafunzi angalau wa skuli.

84. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Ujenzi wa barabara ya Mtambile hadi Kangani umekuwa ukiendelea katika hali ya kusuasua licha ya juhudi za mfano zinazochukuliwa na Serikali yetu ya kuuingiza ujenzi wa barabara kwenye mpango wa bajeti ya Serikali. Barabara hiyo ipo katika hali ngumu kimatumizi inayowafanya wananchi wa Mtambile kushindwa kuitumia ipasavyo barabara hiyo kwa kuhofia kuharibu vyombo na mali zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka utakaohakikisha ujenzi huo unakamilika.

141. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ujenzi wa barabara ya Chake - Wete yenye urefu wa kilomita 22.1 unaendelea, ingawa kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuhusu kutolipwa fidia zao hadi sasa.

(a) Je, ni wananchi wangapi ambao tayari wameshapokea fidia zao tangu kuanza kwa zoezi la kupisha ujenzi wa barabara hii.

(b) Ni idadi gani ya wananchi ambao bado hawajapokea fidia zao hadi sasa na Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi hawa wanapata fidia zao stahiki kwa kupisha ujenzi wa barabara hii.

(c) Serikali inatumia njia gani za tathmini ya mali (majengo) ili kuhakikisha malipo ya fidia yanafanyika kwa haki na kwa usahihi kwa wananchi wanaopisha miradi ya ujenzi wa barabara kama hii ya Chake – Wete.

## III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:</u>**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**19 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**